

KULEA KIZAZI CHA KESHO KWA AJILI YA MAISHA YA KANISA

Sehemu ya Tatu

Umuhimu wa kazi ya Watoto katika Kanisa

Maandiko:Kumb.6:7-9;Mith.22:6;2 Tim.3:15;Mate.16:31,1:14;Warum.12:12

I.Siku zilizopita hatukuzingatia kazi ya watoto;hata hivyo,iwapo watoto hawataendelea katika masomo itakuwa ni vigumu kuwa na jamii iliyo bora-angalia foot note Kumb.6:7;11:18-20; Mith.22.6;Waef.6:4;2 Tim.3:15.

II.Mwanzoni, mkutano wa watoto ulikuwa ni wakuhudumia watakatifu waliowaleta watoto katika mkutano;huduma ya kutunza watoto;hatimaye,jambo la kuwatayarisha walimu likatokea,na tukatengeneza vitabu vya kutumia.

A.Kutokana na uzoelevu wetu tunahisi ya kwamba kazi ya watoto ni muhimu sana;kazi ya watoto haifai iwe tu ya kuwaangalia watoto wakati watakatifu wanahudhuria mikutano.

B.Kazi ya watoto iko na jukumu lingine,yaani,kukuza na kulea kizazi chetu cha kesho,tunastahili kuwa waangalifu na kulichunguza jambo hili.

III.Kazi ya watoto iko na jukumu la ziada,ambalo ni kupata jamii za hao watoto- Mat.16:31;--angalia foot note.Kut.12:3-4;Mwa.7:1.

A.Watoto hupenda kutengeneza urafiki;haswa ni rahisi kwa watoto walio na umri kati ya miaka sita na miaka kumi na mbili kupata marafiki, na wanawasikiza marafiki zao:

1.Kwa hivyo ni rahisi mtoto kumuongoza mtoto mwenzake;watoto wanapoimba nyimbo pamoja,injili inafanya kazi na inaenea kutoka kwa mtoto mmoja hadi mwingine

2.Hata hivyo,lengo letu, haliwalengi watoto pekee,bali pia kupitia kwa watoto,tunataka kuwafikia wazazi wao na pia ndugu na dada zao.

B.Kutokana na hili tunaeza kuona umuhimu wa kazi ya watoto;kazi ya watoto inahusika pakubwa na ukuaji wa kanisa.

IV.Hakuna njia ya uhakika ya kutekeleza kazi ya watoto;hakupaswi kuwa na njia moja ya kutekeleza kazi ya watoto.

A.Tunafaa kuwa na mahali tofauti tofauti kwa ajili ya watoto,mikutano inaweza kuandaliwa kwa wakati tofauti tafauti na tunaweza kutumia njia tofauti tofauti kuandaa mikutano ya watoto,ni sharti tuwe na malengo tofauti,na vitabu vya mafunzo vinafaa kuzungumzia mambo tofauti tofauti:

1.Kuwa na mahali pengi- Mikutano yao inafaa kuwa katika sehemu nyingi;kila mtakatifu ni sharti afungue nyumba yake na awe na mkutano wa watoto nyumbani mwake.

2.Vifaa vya kutumia- Tumefikiria kutumia kanda za video,ambazo makanisa mengine yanatumia;tunataka kutengeneza kanda ya video ambayo inaonyesha watoto kutoka inchi mbali mbali wakivaa mavazi ya kitamaduni na kuimba nyimbo.

3. Kuwa na malengo mengi- Tunaeza pia kuwaendea wazazi wa watoto na kuwahubiria injili na pia ndugu na jamaa; hii ndio kanuni ya kazi yetu ya injili; zaidi tunapokutana na watu wengi, ndivyo ilivyo bora.

4. Kuwa na njia nyingi- Nyumba zilizo na watoto zinaweza kuchukuwa jukumu la kufungua makao yao na kuwauliza watoto wao wakaribishe watoto wengine wa majirani; kisha watoto wanaweza kuzitazama kanda za video, wakisisikiliza hadithi, hii ndio njia ya kuandaa mkutano ya watoto mara moja kwa wiki.

5. Kuwa na wakati tofauti- Ni bora kuwa na nyakati tofauti tofauti kwa ajili ya mikutano ya watoto; ratiba ni sharti iwe legevuni; tunahitaji kutumia wakati ambapo watoto wametoka shuleni kuandaa mikutano ya watoto.

B. Njia ya kutekeleza kazi ya watoto hutegemea wandugu kuchukuwa uongozi katika kazi ya watoto.

1. Tusitengeneze mipangilio maalumu ya kutafuta walimu kwa ajili ya mikutano ya watoto katika nyumba za mikutano; badala yake tutafute idadi fulani ya wandugu na wadada wachanga ambao wanahudhuria mikutano mara kwa mara; aina hii ya huduma haitaji watu wengi.

2. Tunahitaji kutayarisha mafunzo kwa ajili ya mikutano ya watoto; tusiandae mikutano ya watoto bila kujitayarisha:

a. Wandugu ambao wanaongoza katika kazi ya watoto wanahitaji kuandika na kutayarisha mafunzo; lakini watakatifu wanafaa kuamua njia iliyo bora ya kutumia hayo mafundisho.

b. Iwapo kuna watakatifu ambao wamepewa jukumu la kutayarisha mafunzo, basi watakatifu (wanaofundisha watoto) hawaitaji kufanya kazi kubwa; tunaweza kupeana kanuni za kufuatwa katika kazi ya watoto; ni juu ya watakatifu wenyewe kujua namna ya kutekeleza.

3. Mikutano ya watoto iandaliwa katika sehemu nyingi, nyakati tofauti tofauti, na kutumia njia tofauti; hili linahitaji ushirikiano wa kila mtu- Mat 1:14; Wakol. 4:2; Warum. 12:12.